JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI ILEJE,
S.L.P 124,
**ILEJE – SONGWE**
15/05/2018

SIMU NO.
MKUU WA SHULE: 0757**-579877**
MAKAMU MKUU WA SHULE: **0756-659363**
MATRON/PATRON………………………..
MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI …………………………..
…………………………………………………………………….
S.L.P………………………………………**.**
………………………………………………**.**

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILEJE HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE MKOA WA SONGWE MWAKA 2018.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahususi ya…………… shule ya sekondari Ileje ipo umbali wa km 04 Kutokea makao makuu ya Wilaya Kusini mwa kijiji cha Itumba usafiri wa basi kutoka mjini Ili uweze kufika shuleni ukitokea STANDI KUU Mbeya, utapanda gari zinazoenda Tunduma na kushuka standi ya Mpemba. Ukitokea DSM utapanda gari zinazoenda Tunduma na utashukia standi ya Mpemba. Kwa wale wanaotoka njia ya Sumbawanga nao watashukia standi ya Mpemba. Kutoka standi ya Mpemba utapata usafiri wa kwenda Itumba ambayo ndiyo makao makuu wa wilaya ya Ileje. Aidha upo usafiri wa moja kwa moja kutoka Mbeya (Stendi Kuu) ambapo kuna Bus la moja kwa moja hadi shuleni mabasi hayo yameandikwa SMART BUS. Ukifika mji wa Isongole Uliza au omba kushukia shule ya sekondari Ileje nauli ni shilingi 6000/= kwa Bus hilo la SMART BUS.

Mhula wa masomo unaanza tarehe 02**/07/2018** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2018 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 08/07/2018.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya shule

**A. WAVULANA**

**a) Suruali 2, moja rangi ya kahawia (brown) na ya pili iwe rangi nyeusi vitambaa. Suluari zinapatikana shuleni kila moja shilingi elfu ishirini na tano tu. (25,000/=).**

**NB:** Kuepuka tofauti ya rangi hasa brown suluari zote utazikuta shuleni.

**b)** Mashati 2 yote rangi nyeupe mikono mirefu yawe marefu ya kuweza kuchomekea kwenye suruali vizuri (uje nayo).
**c)** Tai 2 ndefu rangi ya vitambaa vya suruali hapo juu.( zinapatikana shuleni kila moja shilingi 5,000/=)
**d)** Viatu vya ngozi, jozi 2 vyenye visigino vifupi na vya kamba na pia visiwe na mapambo aina yoyote.
**e)** Soksi rangi nyeusi jozi mbili
**f)** Sweta rangi ya bluu (blue) iliyoshonwa vizuri yenye mchongo wa V shingoni
**g)** Mkanda mweusi wa ngozi .


**B. WASICHANA**

**a)** Sketi 2 moja rangi ya kahawia (brown) na ya pili iwe nyeusi. , shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu (**sketi utazikuta shuleni kwa shilingi 25,000/= kila moja)**
**b)** Sweta rangi ya bluu iliyoshonwa vizuri yenye shingo ya "V."
**c)** Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi, vya kamba na visiwe na mapambo yoyote.
**d)** Tai mbili ndefu rangi ya kitambaa cha sketi za hapo juu. (zinapatikana shuleni kila moja shilingi elfu tano tu (5,000/=)
**e)** Soksi ndefu rangi nyeupe jozi mbili.

NB: Aidha lipo vazi la kazi za nje maarufu kwa "Shamba dress" ambalo huvaliwa na wanafunzi wanapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo na pia vazi hilo hutumika kama nguo anayovaa akiwa shuleni, sare hizo zishonwe kwa mashono yaliyoonyeshwa katika michoro hii hapa chini idadi ya aina hiyo ya sare zisipungue mbili (02).

**A. WASICHANA**

- Truck suit rangi ya blue yenye mistari ya njano au nyeupe
- Gauni draft ndogo ndogo zenye rangi ya kijani na nyeupe (angalia mfano wa kitambaa kimeambatanishwa na barua hii).




Gauni la kuvaa wakati wa kazi na usio wa kazi maeneo ya shule (shamba dress) gauni liwe refu mpaka kwenye kifundo.

- ❖ T-shirt yenye colar na rangi ya njano Nembo ya shule (Tsh.16, 000/=) zinapatikana hapa shuleni.

**B. WA VULANA**

- ❖ Truck suit rangi ya blue yenye mistari ya njano au nyeupe.
- ❖ Suruali khaki mbili (2) – mashono kama suruali ya sare ya shule.
- ❖ T-shirt rangi ya njano yenye kola na Nembo ya shule (Tsh.16, 000/=) zinapatikana hapa shuleni.

NB:

- ❖ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za ziada/ kuvaa au kupatikana na mavazi ya aina nyingine yoyote ya kiraia nje na sare au shamba dress au track suit kama ilivyoainishwa hapo juu.
- ❖ Atakayepatikana na mavazi tofauti na hapo juu akiwa amevaa shuleni na au amezitunza Bwenini atapewa adhabu kali na kuziteketeza nguo hizo yeye mwenyewe.

2.2 Ada na michango ya shule

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **kupitia Benki ya NMB Account No. 60801200054 ILEJE SEKONDARI RECURENT EXPENDITURE( tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)**

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(i) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

(ii) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kulipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

**NB:**Fedha ya Taaluma,wapishi,walinzi na vibarua wengine ilipwe kwenye akauti ya Ada (**NMB Account No. 60801200054 ILEJE SEKONDARI RECURENT EXPENDITURE)**

(iii) Shilingi 15,000/= kwaajili ya ukarabati wa samani

(iv) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitabulisho na picha

(v) Shilingi 10,000/= kwaajili ya Afya

(vi) Shilingi 5,000/= (Mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya),Inamuhusu mwanafunzi ambaye hana Bima ya NHIF.

(vii) Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima Mock

(viii) Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

**NB:**Fedha ya ukarabati,kitambulisho,Nembo,afya,Bima, mock na tahadhari ilipwe kwenye akauti (**NMB Account No. 60810002998 ILEJE SEKONDARI PROJECT ACOUNT)**

Angalizo jumla ya ada na michango kwa wanafunzi wa:-

(i) Bweni ni shilingi 183,000/=

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

(i) Laboratory coat (kwa wanafunzi wote wa Sayansi)
(ii) Ream ya karatasi A4 - 1 (kwa mwaka)
(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
(iv) Dissective kit kwa wanafunzi wa Biolojia (itakaguliwa).
(v) Scientific calculator
(vi) Godoro ft $2\,^1/_2$
(vii) Mashuka pair 2 (rangi ya bluu bahari), blanketi 1, foronya1(bluu bahari) chandarua 1
(viii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
(ix) Ndoo mbili mbili kubwa 1(lita 20) na ndogo 1 (lita 10)
(x) kwanja1, jembe1,(kwa wote)
PCM – Mfagio mgumu 1(Hand broom)
PCB – Mfagio laini 1(Soft broom)
HGK – Dekio 1 (Mopper)
HGL – Driyer / Squzer 1
HKL – Shoka 1 (lenye mpini).

## 3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa/ utoro
(iii) kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lungha chafu kwa mwanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa miba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

4. Viambatisho na fomu muhimu
   (a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (medica Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
   (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai
   (c) Fomu ya mzazi kukuri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
   (d) Picha nne (4) za wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu
5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

*KARIBU SANA KATIKA SHULE HII*

**....................**

JULITHA MWAULAMBO

MKUU WA SHULE

SCHOOL MOTTO “LET US AIM FAR”